MARKETINGLINK TANZANIA LIMITED

SERA YA FARAGHA NA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Tarehe ya Kuanza Kutumika: 09/09/2026
Toleo la Hati: KWANZA

1. UTANGULIZI

MarketingLink Tanzania Limited inatambua umuhimu wa kulinda faragha na taarifa binafsi za wateja, washirika, wafanyakazi, washiriki wa programu, watumiaji wa huduma na watu wengine ambao taarifa zao zinaweza kuchakatwa katika utekelezaji wa shughuli za Kampuni.

Sera hii inaeleza namna MarketingLink inavyokusanya, kutumia, kuhifadhi, kulinda na pale inapohitajika, kushirikisha taarifa binafsi katika utekelezaji wa shughuli na huduma zake.

MarketingLink inajitahidi kuhakikisha kuwa uchakataji wa taarifa binafsi unafanyika kwa njia ya uwajibikaji, uwazi, usalama na kwa madhumuni halali, kwa kuzingatia sheria na matakwa ya kisheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

2. MADHUMUNI YA SERA

Madhumuni ya Sera hii ni:

i. kuweka misingi ya namna MarketingLink inavyoshughulikia taarifa binafsi
ii. kueleza kwa uwazi aina ya taarifa zinazoweza kukusanywa
iii. kueleza madhumuni ambayo taarifa hizo hutumika
iv. kuweka misingi ya ulinzi na usalama wa taarifa
v. kueleza haki za wahusika wa taarifa binafsi, na
vi. kuweka utaratibu wa kushughulikia masuala yanayohusiana na faragha na ulinzi wa taarifa.

3. MAANA YA TAARIFA BINAFSI

"Taarifa binafsi" ni taarifa zinazomhusu mtu ambaye ametambuliwa au anaweza kutambuliwa moja kwa moja au kwa kuhusianishwa na taarifa nyingine.
Kulingana na aina ya huduma au uhusiano uliopo kati ya MarketingLink na mhusika, taarifa hizo zinaweza kujumuisha:

i. Jina kamili
ii. Namba ya simu
iii. Anwani ya barua pepe
iv. Anwani ya makazi au mawasiliano
v. Taarifa za taasisi au kampuni
vi. Cheo au taarifa za kitaaluma
vii. Taarifa za utambulisho pale inapohitajika kisheria au kiutendaji
viii. Taarifa zinazotolewa kupitia fomu, tafiti au dodoso
ix. Taarifa za ushiriki katika kampeni, matukio au programu
x. Mawasiliano kati ya mhusika na MarketingLink
xi. Mapendeleo ya mawasiliano
xii. Taarifa za matumizi ya mifumo ya kidijitali, na

Taarifa nyingine zinazohitajika kwa madhumuni halali na yaliyobainishwa.

MarketingLink haitakusanya taarifa binafsi zisizo za lazima kwa madhumuni yaliyokusudiwa isipokuwa pale ambapo kufanya hivyo kunaruhusiwa au kutakiwa na sheria.

4. NAMNA TUNAVYOKUSANYA TAARIFA

MarketingLink inaweza kukusanya taarifa binafsi kupitia:

i. Taarifa zinazotolewa moja kwa moja na mhusika
ii. Matumizi ya tovuti, mifumo au majukwaa ya kidijitali ya Kampuni
iii. Usajili wa matukio, programu, kampeni au shughuli nyingine
iv. Tafiti na dodoso
v. Mawasiliano ya simu, barua pepe au njia nyingine za mawasiliano
vi. Wateja, washirika au taasisi tunazofanya nazo kazi, pale ambapo ukusanyaji au uhamishaji huo unaruhusiwa kisheria
vii. Vyanzo vya taarifa vinavyopatikana hadharani, pale ambapo matumizi yake yanaruhusiwa kisheria, na

Njia nyingine halali zinazohusiana na shughuli za Kampuni.

5. MADHUMUNI YA MATUMIZI YA TAARIFA

MarketingLink inaweza kutumia taarifa binafsi

kwa madhumuni yafuatayo:

i. Kutoa na kusimamia huduma

ii. Kusimamia mahusiano na wateja na washirika
iii. Kuwasiliana na wateja, washiriki na wadau;
iv. Kutekeleza kampeni za masoko na mawasiliano
v. Kufanya tafiti za soko
vi. Kufanya uchambuzi wa mahitaji na mwenendo wa hadhira
vii. Kusimamia matukio, activations na programu
viii. Kuboresha huduma na mifumo ya Kampuni
ix. Kushughulikia maombi, maswali na malalamiko
x. Kusimamia mikataba, malipo na kumbukumbu za biashara
xi. Kuzuia matumizi mabaya, udanganyifu au shughuli zisizo halali
xii. Kutekeleza wajibu wa kisheria na kikazi, na
xiii. Kulinda maslahi halali ya Kampuni pale ambapo sheria inaruhusu.

Taarifa binafsi hazitatumika kwa madhumuni yasiyohusiana kwa kiasi kikubwa na madhumuni ambayo taarifa hizo zilikusudiwa bila kuwa na msingi halali wa kufanya hivyo.

6. MSINGI WA KISHERIA WA UCHAKATAJI

MarketingLink itachakata taarifa binafsi kwa msingi unaotambuliwa na sheria husika.

Msingi huo unaweza kujumuisha:

i. Ridhaa ya mhusika
ii. Ulazima wa kutekeleza mkataba au hatua zilizoombwa kabla ya mkataba
iii. Kutekeleza wajibu wa kisheria
iv. Kulinda maslahi muhimu ya mhusika pale inapohusika
v. Maslahi halali ya Kampuni pale ambapo inaruhusiwa kisheria, au
vi. Msingi mwingine unaotambuliwa na sheria.

Pale ambapo uchakataji unategemea ridhaa, mhusika anaweza kuondoa ridhaa hiyo kwa mujibu wa taratibu na mipaka inayoruhusiwa na sheria.

7. MATUMIZI YA TAARIFA KWA MASOKO NA MAWASILIANO

MarketingLink inaweza kutumia taarifa binafsi kwa madhumuni ya mawasiliano ya kibiashara, kampeni, matangazo, tafiti, matukio na shughuli nyingine za masoko pale ambapo kufanya hivyo kuna msingi halali.

Pale ambapo sheria inahitaji ridhaa, MarketingLink itatafuta ridhaa husika kabla ya kufanya mawasiliano ya moja kwa moja ya kimasoko.
Mhusika anaweza kuomba kuondolewa katika mawasiliano ya kimasoko kwa kutumia utaratibu

wa kujiondoa (unsubscribe) au kuwasiliana na Kampuni.

8. USHIRIKISHAJI WA TAARIFA NA WAHUSIKA WENGINE

MarketingLink inaweza kushirikisha taarifa binafsi kwa kiwango kinachohitajika na kinachoruhusiwa kisheria na:

i. Wafanyakazi na wawakilishi walioidhinishwa
ii. Washauri wa kitaalamu
iii. Watoa huduma za teknolojia
iv. Wakandarasi na consultants
v. Washirika wa kampeni au programu
vi. Wateja, pale ambapo ni sehemu ya huduma iliyokubaliwa
vii. Watoa huduma za malipo au huduma za kiutawala
viii. Mamlaka za Serikali au vyombo vya sheria pale inapohitajika kisheria, na

Wahusika wengine pale ambapo mhusika ametoa idhini au sheria inaruhusu.
MarketingLink itachukua hatua zinazofaa kuhakikisha kuwa wahusika wanaopokea au kuchakata taarifa kwa niaba yake wanazingatia wajibu wa usiri, usalama na ulinzi wa taarifa.

9. UHAMISHAJI WA TAARIFA NJE YA TANZANIA

Endapo taarifa binafsi itahitaji kuhifadhiwa, kuchakatwa au kuhamishwa kwenda nje ya Tanzania, MarketingLink itazingatia matakwa ya sheria yanayohusiana na uhamishaji huo na, pale inapohitajika, kuweka hatua na kinga stahiki za kisheria na kiusalama.

10. USALAMA WA TAARIFA

MarketingLink itaweka hatua zinazofaa za kiufundi, kiutawala na kiutendaji kwa ajili ya kulinda taarifa binafsi dhidi ya:

i. Upatikanaji usioidhinishwa
ii. Matumizi yasiyoruhusiwa
iii. Ufunuo usioidhinishwa
iv. Upotevu
v. Uharibifu
vi. Mabadiliko yasiyoruhusiwa, na
vii. Uchakataji mwingine usio halali.

Hatua hizo zinaweza kujumuisha udhibiti wa upatikanaji, uthibitishaji wa watumiaji, usimamizi wa ruhusa, usiri wa taarifa, usalama wa mifumo na taratibu za ndani za Kampuni. Hata hivyo, hakuna mfumo wa kiteknolojia unaoweza kuhakikishwa kuwa salama kwa asilimia mia moja dhidi ya kila aina ya tishio.

11. UHIFADHI WA TAARIFA

MarketingLink itahifadhi taarifa binafsi kwa muda unaohitajika kwa madhumuni ambayo zilikusanywa au kwa muda unaotakiwa au kuruhusiwa kisheria.

Muda wa kuhifadhi unaweza kuathiriwa na

i. Madhumuni ya ukusanyaji
ii. Aina ya taarifa
iii. Masharti ya mkataba
iv. Wajibu wa kisheria na udhibiti
v. Mahitaji ya kumbukumbu za biashara
vi. Migogoro au madai ya kisheria, na
vii. Mahitaji halali ya kiutendaji ya Kampuni.

Taarifa ambazo hazihitajiki tena zitafutwa, kuharibiwa au kufanywa zisizomtambulisha mhusika kwa njia salama, kwa kuzingatia matakwa ya sheria.

12. HAKI ZA MHUSIKA WA TAARIFA

Kwa mujibu wa sheria husika, mhusika anaweza kuwa na haki ya:

i. kupata taarifa kuhusu namna taarifa zake zinavyochakatwa
ii. kuomba kupata taarifa binafsi zinazomhusu
iii. kuomba marekebisho ya taarifa zisizo sahihi au zisizokamilika
iv. kuomba kufutwa kwa taarifa pale ambapo sheria inaruhusu
v. kupinga aina fulani za uchakataji
vi. kuondoa ridhaa pale ambapo uchakataji unatokana na ridhaa
vii. kuomba kuwekwa kwa vikwazo katika uchakataji pale ambapo sheria inaruhusu, na
viii. kuwasilisha malalamiko kwa mamlaka husika ya ulinzi wa taarifa binafsi.

Maombi yanaweza kuhitaji uthibitisho wa utambulisho na yanaweza kuwa chini ya mipaka au masharti yanayotambuliwa na sheria.

13. TAARIFA ZA WATOTO NA VIJANA

MarketingLink haitakusanya kwa makusudi taarifa binafsi za watoto isipokuwa pale ambapo ukusanyaji huo ni halali au una madhumuni halali na umefanyika kwa kuzingatia matakwa ya sheria na kinga zinazohitajika.

Katika utekelezaji wa programu zinazohusisha wanafunzi au vijana, MarketingLink inaweza kuweka hatua za ziada za ulinzi kulingana na aina ya programu na mahitaji ya kisheria.

14. USHIRIKISHAJI WA TAARIFA KATIKA HUDUMA ZA WATEJA

Pale ambapo MarketingLink inatekeleza huduma kwa niaba ya mteja wake na huduma hiyo inahusisha taarifa binafsi za watu wengine, majukumu ya kila upande kuhusu ukusanyaji, matumizi, uhifadhi, usalama na ulinzi wa taarifa yataainishwa katika mkataba husika au Data Processing Agreement, pale inapohitajika.

15. UHALALI NA USAHIHI WA TAARIFA

MarketingLink itachukua hatua zinazofaa kuhakikisha kuwa taarifa binafsi zinazotumika ni sahihi na pale inapohitajika zinaendelea kuwa za kisasa.

Mhusika anahimizwa kutoa taarifa sahihi na kuwasiliana na Kampuni endapo taarifa zake zinahitaji kusahihishwa.

16. MATUKIO YA UVUJISHAJI AU UVUNJIFU WA USALAMA WA TAARIFA

MarketingLink itaweka taratibu za kutambua, kuchunguza, kudhibiti na kushughulikia matukio yanayoweza kuhatarisha usalama wa taarifa binafsi.

Endapo kutatokea uvunjifu wa usalama wa taarifa unaohitaji taarifa kwa mujibu wa sheria, MarketingLink itachukua hatua zinazohitajika ndani ya mfumo wa kisheria na udhibiti unaotumika.

17. COOKIES NA TEKNOLOJIA ZA KIDIJITALI

Tovuti au mifumo ya kidijitali ya MarketingLink inaweza kutumia *cookies* na teknolojia zinazofanana kwa madhumuni kama:

i. Kuendesha na kuboresha utendaji wa tovuti
ii. Kuchanganua matumizi ya tovuti
iii. Kuboresha uzoefu wa mtumiaji
iv. Kupima ufanisi wa kampeni
v. Kuchanganua trafiki, na
vi. Kusaidia shughuli halali za masoko ya kidijitali.

Mtumiaji anaweza kuwa na uwezo wa kudhibiti cookies kupitia mipangilio ya kivinjari au kifaa chake.

18. TOVUTI NA HUDUMA ZA WAHUSIKA WENGINE

Mifumo au mawasiliano ya MarketingLink yanaweza kuwa na viunganishi vinavyoelekeza kwenye tovuti au huduma za wahusika wengine.
MarketingLink haiwajibiki moja kwa moja kwa sera za faragha, usalama au matumizi ya taarifa zinazotekelezwa na wahusika hao. mtumiaji anashauriwa kusoma sera ya faragha ya mhusika wa tatu kabla ya kutoa taarifa binafsi.

19. UZINGATIAJI WA SHERIA

MarketingLink itazingatia sheria na kanuni zinazotumika kuhusu ulinzi na uchakataji wa taarifa binafsi nchini Tanzania.
Sera hii itatafsiriwa pamoja na matakwa mengine ya kisheria, kanuni, miongozo au maagizo ya mamlaka yenye mamlaka juu ya ulinzi wa taarifa binafsi.

20.MABADILIKO YA SERA

MarketingLink inaweza kurekebisha Sera hii mara kwa mara ili kuakisi mabadiliko ya:

i. Sheria na kanuni
ii. Huduma za Kampuni
iii. Teknolojia
iv. Mifumo ya biashara, au
v. Taratibu za ulinzi wa taarifa.

Toleo jipya litaonyesha tarehe ya kuanza kutumika na litapatikana kupitia njia zinazofaa za mawasiliano za Kampuni.

21. MAWASILIANO YA MASUALA YA FARAGHA

Kwa maswali, maombi, malalamiko au taarifa zinazohusiana na faragha na ulinzi wa taarifa binafsi, wasiliana na:

MARKETINGLINK TANZANIA LIMITED

Barua pepe: info@marketinglink.co.tz
Simu: +255722 577 809
Tovuti: www.marketinglink.co.tz

© MarketingLink Tanzania Limited.

22. SHERIA INAYOTUMIKA

Sera hii itaongozwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwemo sheria inayosimamia ulinzi wa taarifa binafsi pamoja na kanuni na matakwa mengine ya mamlaka husika.

MARKETINGLINK TANZANIA LIMITED

Faragha. Uaminifu. Uwajibikaji. Ulinzi wa Taarifa.